

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe,

Ofisi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar imepokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kuhusiana na “Kufukuzwa Uanachama wa Chama cha Mapinduzi Ndg. Abdalla Maulid Diwani” Mwakilishi wa Jimbo Jang’ombe, yenye kumbukumbu Namba MVW/26/HQ3/43 ya tarehe 30 Mei, 2018.


Barua hiyo imeeleza kuwa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Mjini iliyokutana tarehe 5 Aprili, 2018 imemfukuza uanachama Mheshimwa Abdalla Maulid Diwani – Mwakilishi wa Jimbo la Jang’ombe chini ya Ibara ya 89(14) ya Katiba ya CCM Toleo la 2017 baada ya kuthibitisha tuhuma za ukiukwaji wa Kanuni za Uongozi na Maadili za CCM.

Kufuatia uamuzi huo, Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM iliyokutana tarehe 28 – 29 Mei, 2018 iliridhia uamuzi huo na

hivyo, ilimfukuza katika uongozi wa CCM Mwakilishi huyo chini ya Ibara ya 102(21) ya Katiba ya Chama hicho.

Kutokana na maamuzi hayo na kwa mujibu wa kifungu cha 71(1)(a) kikisomwa pamoja na kifungu cha 68(d) vya Katiba ya Zanzibar, 1984, Mjumbe Mwakilishi huyo amekosa sifa ya kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha 71(2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, naomba kutoa taarifa rasmi kwamba Kiti cha Mjumbe Mwakilishi cha Jimbo la Jang'ombe, kipo wazi.

Ahsanteni,



Zubeir Ali Maulid,

Spika,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar.